K


# MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA



JARIDA LA HALI YA HEWA KILIMO

*Na. 23. Msimu wa Kilimo 2021/22* *Tathmini, Mei 1-10, 2022 na Matazamio kwa Kipindi cha Mei 11-20, 2022*


**MUHTASARI**

- Hali ya ukavu inayotarajiwa itasaidia shughuli za uvunaji na ukaushaji wa mazao.
- Wafugaji wanashauriwa kukusanya majani na chakula cha mifugo na kuvihifadhi vizuri kwa ajili ya matumizi ya baadae, pia kupata ushauri wa maafisa ugani juu ya utunzaji bora wa mifugo kwa kuzingatia hali ya hewa inayotarajiwa.
- Wakulima wanashauriwa kuendelea na shughuli za utunzaji wa mashamba na matumizi ya pembejeo kwa kufuata ushauri wa maafisa ugani.


## MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA MEI 1-10, 2022

Katika dekadi hii. migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) ilionekana kuimarika wakati ile ya kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) ilionekana kupungua nguvu. Hali hii iliendelea kuruhusu ukanda mvua (ITCZ) kusogea kuelekea upande wa kaskazini mwa nchi kuimarisha mifumo ya mvua katika maeneo hayo.

Katika eneo la kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (pwani ya Angola), joto la bahari lilikuwa la juu kidogo ya wastani, hivyo kuwa na mchango hafifu katika kusukuma upepo wenye unyevunyevu kutoka misitu ya Congo kuelekea maeneo ya magharibi mwa nchi. Joto la bahari katika upande wa magharibi mwa bahari ya Hindi (pwani ya Afrika Mashariki) lilikuwa la wastani wakati lile la upande wa mashariki mwa bahari ya Hindi (Indonesia) lilikuwa juu kidogo ya wastani hadi wastani. Hali hii ilisababisha upepo wenye unyevunyevu kuvuma kutoka baharini kuelekea katika maeneo ya mashariki mwa nchi kwa baadhi ya nyakati

## TATHMINI YA MVUA KATIKA KIPINDI CHA MEI 1-10, 2022

Katika kipindi hiki, maeneo mengi nchini yalipata vipindi vya ukavu wakati maeneo machache yalipata vipindi vichache vya mvua chini ya 26 mm. Hata hivyo, maeneo machache yanayozunguka ziwa Victoria yalipata mvua nyingi hususan katika mkoa wa Mara kama inavyoonekana kwenye kielelezo.




Kielelezo: Kiasi cha mvua katika kipindi cha Mei 1-10, 2022

## TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA MEI 1-10 2022

Vipindi vichache vya mvua zilizonyesha katika maeneo yanayopata mvua za msimu zimesaidia ukuaji wa mazao na malisho kwa ajili ya wanyama. Kwa upande wa maeneo yanayopata mvua mara mbili kwa mwaka, ukosefu wa mvua za kutosha umedhihirika katika maeneo mengi na kusababisha upungufu wa unyevunyevu katika udongo na kuathiri mazao.

Kwa maeneo mengi yanayopata mvua za msimu, mazao ya mahindi yako katika hatua ya kukomaa na kukauka isipokuwa katika mkoa wa Njombe ambako mahindi yapo katika hatua za mwanzo za kukomaa na wakulima katika maeneo hayo waliendelea na utunzaji wa mashamba, ikiwa ni pamoja na kudhibiti wadudu waharibifu na magonjwa ya mimea.

Kwa ujumla, mazao ya mahindi na mpunga yalikuwa katika hali nzuri

Hata hivyo mazao ya alizeti, choroko, kunde, mbaazi na mtama yameonekana kuwa katika hali ya wastani katika maeneo mengi nchini.

Maeneo yanayozunguka Ziwa Victoria, zao la mahindi lilikuwa katika hatua ya kubeba. Unyeshaji hafifu wa mvua kwa maeneo mengine kama nyuanda za juu kaskazini mashariki na Pwani ya kaskazini umeathiri

kilimo cha mahindi. Wakulima hususan katika mikoa ya Pwani, Dar es Salaam na Kagera wanajishughulisha na uvunaji mihogo.
Hali ya maji na malisho kwa mifugo na wanyamapori ilikuwa ya kawaida maeneo mengi nchini.

## HALI YA MAJI KATIKA KIPINDI CHA MEI 1-10, 2022

Kwa ujumla hali ya maji katika mabwawa, mabonde na mtiririko wa maji kwenye mito ni wa kawaida katika maeneo mengi nchini isipokuwa katika mabonde ya Ziwa Victoria, bonde la Ruvuma na Pwani ya Kusini ambako ongezeko kidogo la maji lilionekana. Hata hivyo, upungufu wa maji umeonekana katika bonde kati.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA MEI 11-20, 2022

Migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia inatarajiwa kuendelea kuimarika wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia inatarajiwa kupungua nguvu. Hali hii itasababisha ukanda mvua (ITCZ) kuendelea kusogea maeneo ya kaskazini mwa nchi.
Joto la bahari katika eneo la kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) linatarajiwa kuwa la wastani hadi chini kidogo ya wastani na hivyo kuendelea kuwa na mchango mdogo katika kusababisha upepo wenye unyevunyevu kutoka misitu ya Congo kuelekea magharibi mwa nchi. Joto la bahari katika upande wa magharibi mwa Bahari ya Hindi linatarajiwa kuendelea kuwa la wastani wakati lile la upande wa mashariki mwa baharí linatarajiwa kuendelea kuwa juu kidogo ya wastani hadi wastani. Hali hii inatarajiwa kuendelea kusababisha upepo wenye unyevunyevu kuvuma kutoka baharini kuelekea katika maeneo ya mashariki mwa nchi.

## HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA MEI 11-20, 2022

Maeneo ya kanda ya Ziwa Viktoria (mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara) yanatarajiwa kuwa na vipindi vya mvua na ngurumo za radi.
Pwani ya kaskazini (mikoa ya Tanga, kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba) na pwani ya kusini (mikoa ya Mtwara na Lindi) yanatarajiwa kuwa na vipindi vichache vya mvua hususani katika nusu ya pili ya dekadi.
Maeneo ya magharibi mwa nchi (mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora) yanatarajiwa kuwa na vipindi vichache vya mvua na ngurumo za radi katika maeneo machache.
Maeneo ya kanda ya kati (mikoa ya Dodoma na Singida) pamoja na nyanda za juu kusini magharibi (mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa) yanatarajiwa kuwa makavu kwa ujumla.
Maeneo ya kanda ya kusini (mkoa wa Ruvuma na kusini mwa Morogoro) yanatarajiwa kuwa makavu kwa kipindi kirefu pia vipindi vichache vya mvua nyepesi vinatarajiwa hususan katika nusu ya kwanza ya dekadi.
Maeneo ya nyanda za juu kaskazini mashariki (mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro) yanatarajiwa kuwa na vipindi vichache vya mvua hususan katika nusu ya pili ya dekadi.

## HALI YA HEWA KILIMO: MATARAJIO NA USHAURI KIPINDI CHA MEI 11-20, 2022

Mvua zinazotarajiwa katika baadhi ya maeneo nchini zitaendelea kuimarisha unyevunyevu kwenye udongo ambao utasaidia ukuaji wa mazao. Hali ya ukavu inayotarajiwa itasaidia shughuli za uvunaji na ukaushaji wa mazao.
Wakulima wanashauriwa kutunza mashamba yao na kufuata ushauri wa maafisa ugani kutoka katika maeneo yao ikiwa ni pamoja na kuendelea na shughuli za upuliziaji dawa kwa wadudu waharibifu hususan katika maeneo yaliyoathiriwa na viwavi jeshi.
Wafugaji nao wanashauriwa kukusanya majani na chakula cha mifugo na kuvihifadhi vizuri kwa ajili ya matumizi ya baadae. Pia wanatakiwa kupata ushauri wa maafisa ugani juu ya utunzaji bora wa mifugo kwa kuzingatia hali ya hewa inayotarajiwa.
Wavuvi wanashauriwa kufuatilia taarifa za hali ya hewa za kila siku ili kufanya maamuzi juu ya wakati sahihi wa kwenda kufanya shughuli za uvuvi.
Kwa ujumla wadau wa kilimo wote wanashauriwa kuendelea kufuatilia taarifa za hali ya hewa kila zinapotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.

## HALI YA MAJI INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA MEI 11-20, 2022

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vinatarajiwa kuwa katika hali ya kawaida katika maeneo mengi nchini. Hata hivyo, watumiaji rasilimali maji wanashauriwa kuitumia kwa uangalifu.

*Jarida limetayarishwa na:*
**Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania**
**Ghorofa ya 3 -Ubungo Plaza – 388 Barabara ya Morogoro,**
*S.L.P 3056; 16102 Dar es Salaam, Simu. 255 -(0) 22 – 2460706-8; Nukushi: 255 - (0) 22 – 2460718 ; Barua pepe: (1) met@meteo.go.tz (2) agromet@meteo.go.tz; Tovuti:*
www.meteo.go.tz, -Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania